

ASb
approved



Barua kwa Mama

Ursula Nafula

Catherine Groenewald

Kiswahili





Mama aliziveka nguo zake katika begi ndogo.



Alinikumbatia akasema, "Kwa heri kwa sasa."




"Mama unaenda wapi?" Nilimwuliza.



Nilianza kulia nikitaka kumfuata.

Baba alinibeba akanituliza.



Baba alisema, "Mamako anaenda hospitalini kujifungua mtoto."



Niliposikia 'mtoto' sikulia tena.


"Kwa nini aende hospitalini?"



Baba alinijibu, "Nitakueleza kwa nini anaenda hospitalini."

Baba alinieleza lakini sikuelewa.

Nilimwuliza, "Ataendelea kunipenda?"



Alinieleza, "Tutakupenda wakati wote."



"Ninaweza kumwandikia barua akiwa huko?" Nilimwuliza
baba.




Jioni hiyo, nilianza kumtungia mama barua.



Nilichukuwa karatasi na kuanza kuandika.



Mama, mama! Baba alisema kwamba umeenda kumleta
mtoto mwingine.



Tafadhali, fanya haraka urudi nyumbani.



Ningependa umlete mtoto msichana.

Nitacheza naye akiwa mkubwa.



Unaweza kuwaleta wawili.

Mmoja atakuwa wangu.



Ninakusubiri hapa nyumbani.



Niliikunja barua yangu ili baba ampelekee mama.

Asubuhi, barua haikuwepo.

You are free to download, copy, translate or adapt this story
and use the illustrations as long as you attribute in the
following way: Ursula Nafula Author - Ursula Nafula

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Catherine Groenewald

Language - Kiswahili

Level - First words © African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

